


# MUONGOZO UNAOHUSU TARATIBU ZA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII-ZANZIBAR

**YALIYOMO**


Yaliyomo ..... i

1. Utangulizi ..... 1
2. Utaratibu wa usajili wa kizazi hai cha ndani ya ndoa ..... 1
3. Taratibu za usajili wa kizazi hai kwa mtoto aliezaliwa nje ya ndoa ..... 2
4. Taratibu za usajili wa tukio la kifo ..... 2
5. Taratibu za usajili wa tukio la ndoa. ..... 3
6. Taratibu za maombi ya cheti cha kutokuwa na kizuizi cha ndoa ..... 4
7. Taratibu za usajili wa tukio la talaka ..... 4
8. Utaratibu wa usajili wa mzanzibari mkaazi ndani ya wakati ..... 5
9. Utaratibu wa usajili wa mzanzibari mkaazi nje ya wakati (kuanzia miaka 25 na kuendelea) 5
10. Sifa za kupewa kadi ya utambulisho wa mzanzibar mkaazi ..... 6
11. Utaratibu wakufuatwa kwa watu wasioridhika na uwamuzi wa sheha ..... 6
12. Taratibu za kufuatwa iwapo kadi ya utambulisho wa mzanzibari mkaazi itapotea au kuharibika ..... 6
13. Maelekezo kwa waliopewa mamlaka ya kufungisha ndoa na kutambua talaka ..... 6
14. Ruhusa ya kubadili taarifa katika cheti cha kuzaliwa, kifo, ndoa, talaka na kitambulisho cha mzanzibari mkaazi ..... 7
15. Taratibu za kufuatwa iwapo cheti kitapotea au kuharibika ..... 7
16. Taratibu za usajili kwa mtoto alieokotwa ..... 7
17. Mahitaji ya hati za viapo au hati za kubadilisha jina(afidavity or deed poll). ..... 7
18. Ngazi(rank) za vyanzo vya taarifa katika kufanya uchunguzi wa taarifa za waombaji wa vyeti vya kuzaliwa nje ya wakati. ..... 8
19. Majadweli ya malipo ya huduma za usajili ya matukio ya kijamii zanzibar ..... 9
    - 19.1 jadweli la malipo ya usajili wa tukio la kizazi ..... 9
    - 19.2 jadweli la malipo ya usajili wa tukio la kifo ..... 9
    - 19.3 jadweli la malipo ya usajili wa tukio la ndoa ..... 10
    - 19.4 jadweli la malipo ya usajili wa tukio la talaka ..... 10
    - 19.5 jadweli la malipo ya usajili wa kitambulisho cha mzanzibari mkaazi ..... 10
20. Hitimisho ..... 11

# MUONGOZO UNAOHUSU TARATIBU ZA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII-ZANZIBAR

## 1. UTANGULIZI

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) ni Taasisi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria No.3 ya mwaka 2018, Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, katika utekelezaji wa Sheria hiyo, Serikali ilitunga Kanuni za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii iliyokuja kufafanua kwa kina juu ya taratibu za usajili wa matukio ya kijamii. Aidha Ofisi imeona ipo haja ya kutoa muongozo kwa Watendaji wote ili kuwawezesha, kuwasaidia pamoja na kuwa na usawa (Uniformity) katika utoaji wa huduma za usajili kwa Wilaya zote, ambapo muongozo huu hautoathiri matakwa ya Sheria No.3/2018, wala Kanuni zake, Sheria No.5 ya mwaka 1985 na marekebisho yake No.4 ya mwaka 2003, pamoja na Sera ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ya mwaka 2007.

## 2. UTARATIBU WA USAJILI WA KIZAZI HAI CHA NDANI YA NDOA

(a) Ikiwa usajili umefanyika kwa wakati ambapo muombaji amepata kipande (Ithibati) cha kuzaliwa kwa Mtoto kutoka Hospitali au kwa sheha ndani ya siku arubaini na mbili (42); vielelezo vitakavyohitajika ni kama vifuatavyo: -

(i) Taarifa ya kuzaliwa kutoka kwa Wakala wa Usajili; yaani kipande cha Hospitali au kwa sheha kwa wale waliojifungua Nyumbani.

(ii) Kivuli cha Kitambulisho au cheti cha kuzaliwa cha Mama, na baba.

(iii) Kivuli cha Cheti cha Ndoa

(iv) Gamba la Kliniki la Mama la vipimo vya ujauzito

**Zingatio:** Kielelezo namba (ii, iii, na iv) vinaweza kutumika kama Muombaji atakuwa anavyo, na kukosekana kwake hakutozuia utowaji wa huduma ya usajili. Isipokuwa Afisa usajili anaweza kuomba uthibitisho mwengine wowote unaoweza kutumika na ambao Muombaji anaweza kuwanao.

(b) Ikiwa tukio la kizazi hai limechelewa kuandikishwa (Late registration) ambapo muombaji hajapata taarifa ya kuzaliwa kutoka Hospitali au kwa sheha ndani ya siku aroubaini na mbili (42); vielelezo vitakavyohitajika ni kama vifuatavyo: -

   (i) Barua ya utambuzi wa kuzaliwa kutoka kwa Sheha wa eneo alilozaliwa muombaji.
   (ii) Kivuli cha Kitambulisho cha mtoa taarifa;
   (iii) Kitambulisho cha muombaji ikiwa ana umri wa miaka kumi na minane (18) na zaidi;
   (iv) Barua ya muombaji kutoka Skuli ya Msingi aliyosoma; barua hiyo ielezee mwaka aliozaliwa, namba ya usajili pamoja na mwaka alioanza darasa la kwanza. Na ikiwa Muombaji hakusoma Skuli, atalazimika kuwasilisha Hati ya kiapo yenye kuthibitisha kutokusoma kwake.
   (v) Picha mbili za pasipoti za Muombaji zilizipingwa hivi karibuni pamoja na picha moja ya mtoa taarifa.

   Afisa usajili anaweza kuomba uthibitisho mwengine wowote unaoweza kutumika ambao muombaji anaweza kuwanao.

## 3. TARATIBU ZA USAJILI WA KIZAZI HAI KWA MTOTO ALIEZALIWA NJE YA NDOA

(a) Mama au mlezi wa mtoto aliezaliwa nje ya Ndoa atapaswa kuomba ruhusa Mahakama ya kadhi au Mahakama ya kawaida (Itategemea na imani ya Muombaji) ili kuweza kutumia jina la Baba ambalo Mahakama hiyo itakuwa imependekeza.

(b) Iwapo atajitokeza Baba ambae ataridhia kutumika jina lake katika cheti cha Mtoto huyo, atalazimika kutumia hati ya kiapo chenye kuthibitisha kuwa ameridhia jina lake litumike na Mama wa mtoto huyo ataridhia kwa kupitia hati ya kiapo,(katika mazingira kama haya kutakuwa na hati za viapo viwili, kimoja cha Baba,na kingine cha Mama)

(c) Pale ambapo baba wa mtoto hapatikani, mtoto ataandikishwa bila jina la baba na mama anaweza kumpa mtoto wake majina yoyote mawili pamoja na jina la kwanza la mtoto na majina hayo yataandikwa kwenye safu ya jina la mtoto;

## 4. TARATIBU ZA USAJILI WA TUKIO LA KIFO

(a) Usajili wa tukio la Kifo ndani ya wakati utafanyika ndani ya siku saba (7) baada ya kutokea kwa tukio hilo. Vielelezo vitakavyohitajika katika usajili wa tukio la kifo ndani ya wakati ni kama vifuatavyo: -

(i) Kibali cha mazishi kutoka Hospital au Sheha wa eneo lilipotokea tukio la kifo.
(ii) Kitambulisho cha mtoa taarifa; na
(iii) Afisa usajili anaweza kuomba uthibitisho mwengine wowote unaoweza kutumika ambao muombaji anaweza kuwanao.

(b) Ikiwa usajili wa tukio la kifo halikusajiliwa ndani ya wakati ambapo muombaji hakupata kibali cha mazishi kutoka Hospitali au kwa sheha ndani ya siku saba (7); vielelezo vitakavyohitajika ni kama vifuatavyo: -

(i) Barua ya uthibitisho wa Kifo kutoka kwa Sheha;
(ii) Hati ya kiapo cha mtoa taarifa kwa uthibitisho wa taarifa za Kifo;
(iii) Kitambulisho cha mtoa taarifa.

Afisa usajili anaweza kuomba uthibitisho mwengine wowote unaoweza kutumika ambao muombaji anaweza kuwanao.

**Zingatio:** Kifo kilichotokea Baharini au kwa sababu ya maafa, uthibitisho wake utatolewa na Afisi ya Kadhi au Mahakamo wa pili wa Raisi

## 5. TARATIBU ZA USAJILI WA TUKIO LA NDOA.

Iwapo muombaji ataomba kusajili Ndoa ndani ya siku 30 baada ya tukio la Ndoa; vielelezo vitakavyohitajika ni kama vifuatavyo: -

(i) Uthibitisho wa Ndoa kutoka kwa Msimamizi wa Ndoa;

(ii) Kwa Mzanzibari Mkaazi, kivuli/ Kopi ya Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi au Kitambulisho kingine chochote rasmi au cheti cha kuzaliwa au barua kutoka kwa Sheha ambapo Ndoa ilifungwa;

(iii) Kwa asiekuwa Mzanzibari Mkaazi, ruhusa ya ukaazi, hati ya kusafiria au kivuli ya Kitambulisho chengine chochote rasmi kutoka nchi anayotoka au barua kutoka kwa Sheha ambapo Ndoa ilifungwa;

Iwapo muombaji ataomba kufanya usajili wa Ndoa nje ya siku 30 baada ya tukio la Ndoa; vielelezo vitakavyohitajika ni kama vifuatavyo

(i) Uthibitisho wa Ndoa kutoka Mahakama ya Kadhi, Kuhani au Mkuu wa Mkoa

(ii) Kwa Mzanzibari Mkaazi, Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi au Kivuli cha Kitambulisho chengine chochote rasmi au cheti cha kuzaliwa au barua kutoka kwa Sheha ambapo Ndoa ilifungwa;

(iii) Kwa asiekuwa Mzanzibari Mkaazi, ruhusa ya ukaazi, hati ya kusafiria au kivuli cha Kitambulisho chengine chochote rasmi kutoka nchi anayotoka au barua kutoka kwa Sheha ambapo Ndoa ilifungwa;

Afisa usajili anaweza kuomba uthibitisho mwengine wowote unaoweza kutumika ambao muombaji anaweza kuwanao.

## 6. TARATIBU ZA MAOMBI YA CHETI CHA KUTOKUWA NA KIZUIZI CHA NDOA

Iwapo Mzanzibari Mkaazi anaeishi Tanzania anatamani kufunga Ndoa katika nchi yeyote ya kigeni kwa mujibu wa Sheria ya nchi hiyo na Sheria ya nchi hiyo inamtaka atoe cheti ambacho kitaonesha hakuna kizuizi cha kisheria katika Ndoa iliyokusudiwa kinachojulikana kwa Wakala, anaweza kutuma maombi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa ZCSRA kwa kupatiwa cheti cha kutokuwa na kizuizi cha Ndoa.

Muombaji atalazimika kuwasilisha Vielelezo vifuatavyo wakati wa kuomba Cheti cha kutokuwa na kizuizi cha Ndoa.

(i) Barua ya sheha wa eneo analoishi yenye kuthibitisha kutokuwepo kwa kizuizi cha Ndoa
(ii) Kivuli cha Kitambulisho chochote cha Muombaji
(iii) Hati ya kiapo cha Mzazi au mlezi chenye kuthibitisha kutokuwepo kwa kizuizi cha Ndoa na;
(iv) Kivuli cha kitambulisho cha chochote cha Mzazi au Mlezi.

Afisa usajili anaweza kuomba uthibitisho mwengine wowote unaoweza kutumika ambao muombaji anaweza kuwanao.

## 7. TARATIBU ZA USAJILI WA TUKIO LA TALAKA

Usajili wa tukio la Talaka utakuwa ndani ya siku 30 baada ya kutangazwa kwa Talaka ambapo Muombaji atalazimika kuwasilisha Vielelezo vifuatavyo wakati wa kuomba Cheti hicho: -

(i) Uthibitisho au amri ya Talaka kutoka kwa mtu au Mahakama ambayo inatambua Talaka;

(ii) Kwa Mzanzibari Mkaazi, kivuli ya Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, kitambulisho cha Taifa cha wahusika au mhusika wa Talaka au cheti cha kuzaliwa au barua kutoka kwa Sheha ambapo Talaka ilitamkwa;

(iii) Kwa asiekuwa Mzanzibari Mkaazi, Kitambulisho cha asiyekuwa Mzanzibari Mkaazi, hati ya kusafiria au Kitambulisho chengine chochote rasmi kutoka nchi anayotoka au barua kutoka kwa Sheha ambapo Talaka ilitamkwa;

(iv) Kivuli cha cheti cha Ndoa ambacho Talaka yake imeombwa kusajiliwa;

Ikiwa usajili wa Talaka utafanyika nje ya wakati wa siku thelathini (30), muombaji atalazimika kuwasilisha vielelezo vifuatavyo;

(i) Uthibitisho wa Talaka kutoka Mahakama ya Kadhi au amri ya Talaka kutoka Mahakamani au mtu aliepewa mamlaka ya kuitambua Talaka;

(ii) Kwa Mzanzibari Mkaazi, kivuli ya Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi cha wahusika au mhusika wa Talaka au cheti cha kuzaliwa au barua kutoka kwa Sheha ambapo Talaka ilitamkwa

(iii) Kwa asiekuwa Mzanzibari Mkaazi, Kitambulisho cha asiekuwa Mzanzibari Mkaazi, hati ya kusafiria au Kitambulisho chengine chochote rasmi kutoka nchi anayotoka au barua kutoka kwa Sheha ambapo Talaka ilitamkwa.

Afisa usajili anaweza kuomba uthibitisho mwengine wowote unaoweza kutumika ambao muombaji anaweza kuwanao.

## 8. UTARATIBU WA USAJILI WA MZANZIBARI MKAAZI NDANI YA WAKATI

Mzanzibari yeyote anaeomba usajili wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ndani ya wakati uliowekwa atalazimika kuwasilisha vielelezo vifuatavyo: -

(i) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa;

(ii) Barua ya Sheha ya eneo analoishi.

(iii) Picha ya Muombaji

Afisa usajili anaweza kuomba uthibitisho mwengine wowote unaoweza kutumika ambao muombaji anaweza kuwanao.

## 9. UTARATIBU WA USAJILI WA MZANZIBARI MKAAZI NJE YA WAKATI (KUANZIA MIAKA 25 NA KUENDELEA)

Mzanzibari Mkaazi yeyote aliyeomba kusajiliwa nje ya wakati atamuandikia barua ya maombi Mkurugenzi Mtendaji wa ZCSRA na kueleza sababu ya maombi yake kwa kuambatanisha vielelezo vifuatavyo: -

(i) Barua ya sheha wa eneo analoishi;

(ii) Kivuli cha Cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa;

(iii) Kivuli cha Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi cha mmoja ya wazazi au mdhamini wake.

Afisa usajili anaweza kuomba uthibitisho mwengine wowote unaoweza kutumika ambao muombaji anaweza kuwanao.

## 10. SIFA ZA KUPEWA KADI YA UTAMBULISHO WA MZANZIBAR MKAAZI

Mtu yeyote anaetaka kuomba au mwenye kuomba kusajiliwa na kupewa Kadi ya utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo

(i) Awe raia wa Tanzania

(ii) Awe Mkaazi wa Zanzibar kwa muda wa miaka kumi (10) mfululizo (sifa hii itatumika kwa watu waliohamia Zanzibar kutoka nje ya Zanzibar.

(iii) Awe mtu mwenye tabia nzuri

(iv) Awe ameingia Zanzibar kihalali na kufuata Sheria na Kanuni zote za Zanzibar

(v) Awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane (18)

(vi) Awe amekusudia kuendelea kuishi Zanzibar.

(vii) Awe na akili timamu

## 11. UTARATIBU WAKUFUATWA KWA WATU WASIORIDHIKA NA UWAMUZI WA SHEHA

Iwapo itatokezea mtu yeyote hakuridhika na uwamuzi wa sheha katika kufuata utaratibu wa usajili anatakiwa kuelekezwa kwenda kulalamika (kukata rufaa) kwa Mkuu wa Wilaya anaehusika. Iwapo uwamuzi huo utakuwa umetolewa na Ofisi (ZCSRA) mwananchi anatakiwa kuelekezwa kukata rufaa kwa Mhe. Waziri anaehusika na Matukio ya Kijamii Zanzibar.

## 12. TARATIBU ZA KUFUATWA IWAPO KADI YA UTAMBULISHO WA MZANZIBARI MKAAZI ITAPOTEA AU KUHARIBIKA

Pale ambapo Kadi ya utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi itapotea au kuharibika, mtumiaji wa Kadi hiyo anatakiwa kutoa taarifa katika Kituo cha Polisi kilichokaribu nae akiambatanisha na barua ya Sheha wa shehia analoishi.

Baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Sheha na kituo cha Polisi na kupokea malipo ya Kadi iliyopotea au kuharibika, Ofisa usajili baada ya kukamilisha taratibu atatoa Kadi mpya ya Mzanzibari Mkaazi.

## 13. MAELEKEZO KWA WALIOPEWA MAMLAKA YA KUFUNGISHA NDOA NA KUTAMBUA TALAKA

Mtu yeyote aliyeruhusiwa au kupewa mamlaka ya kufungisha Ndoa au kutambua Talaka ambaye atakuwa amepokea Madaftari kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji, mara moja kwa Wiki atarejesha katika Ofisi za Wakala za Wilaya vivuli vya ithibati zote (Vivuli vya Tarjis za ndoa na Talaka) za Ndoa au Talaka alizozitoa.

## 14. RUHUSA YA KUBADILI TAARIFA KATIKA CHETI CHA KUZALIWA, KIFO, NDOA, TALAKA NA KITAMBULISHO CHA MZANZIBARI MKAAZI

Mtu yeyote mwenye kuhitaji kubadilisha taarifa katika rejista ya usajili wa Kizazi, Kifo, Ndoa, Talaka na Kitambulisho cha Mzanzibari anatakiwa kuomba kwa Mkurugenzi Mtendaji wa ZCSRA akiambatanisha vielelezo vifuatavyo:

(i) Hati ya kiapo (Affidavity) cha mzazi iwapo mzazi anataka kubadili jina la mtoto wake

(ii) Hati ya kubadisha jina (Deed poll) iwapo muombaji anataka kubadilisha jina lake.

(iii) Kielelezo chengine chochote ambacho kitahitajika na Afisa usajili na ambacho Muombaji atakuwanacho.

**Zingatio:** Marekebisho yoyote yatakayoombwa kufanyika wakati wa kukamilisha usajili, hayotopaswa kulipiwa. Na badala yake Muombaji atalipia ada yakawaida tu.

## 15. TARATIBU ZA KUFUATWA IWAPO CHETI KITAPOTEA AU KUHARIBIKA

Pale ambapo cheti kimepotea au kuharibika, mmiliki anatakiwa kutoa taarifa katika kituo cha polisi kilicho karibu ili kupata barua ya uthibitisho wa hasara au uharibifu kwa cheti hicho.

Baada ya kupokea barua ya uthibitisho wa hasara au uharibifu kutoka Polisi na malipo ya ada inayotakiwa, Afisa Usajili baada ya kuridhika na taratibu stahiki anatoa cheti kipya.

## 16. TARATIBU ZA USAJILI KWA MTOTO ALIEOKOTWA

Mtu aliyemuokota mtoto ambae wazazi wake hawajulikani walipo anatakiwa kutoa taarifa kituo cha polisi kilichokaribu au Sheha aliyekaribu, ambapo Polisi au sheha huyo atatakiwa kumfikisha Mtoto huyo katika Ofisi ya Ustawi wa Jamii, na Ofisi ya Ustawi wa jamii ndio watakao simamia usajili wa kuzaliwa kwa mtoto huyo.

Ikiwa mtoto amezaliwa ndani ya Gereza, Polisi, kituo cha kulelea mayatima, wajibu wa kutoa taarifa za usajili wa mtoto huyo utakuwa ni kwa Ofisa dhamana wa kituo hicho.

Iwapo mtoto amezaliwa ndani ya meli au chombo cha usafiri, Nahodha mkuu wa chombo hicho ndio mwenye dhamana ya kutoa taarifa.

## 17. MAHITAJI YA HATI ZA VIAPO AU HATI ZA KUBADILISHA JINA (AFIDAVITY OR DEED POLL).

Katika usajili wa matukio ya kijamii, hati ya kiapo au hati ya kubadilisha jina itakuwa ikihitajika iwapo: -

(i) Mzazi anataka kubadilisha jina la Mtoto wake aliyechini ya miaka kumi na nane (18)

(ii) Sehemu ya jina la mama au baba lililoandikwa katika cheti cha mtoto limekosewa na linataka kurekebishwa.

(iii) Mtoto amezaliwa nje ya Ndoa na wazazi wake sio waislam na akajitokeza Baba ambae ameridhia jina lake liweze kutumika katika cheti cha mtoto huyo.

(iv) Uhusiano wa Muombaji wa usajili wa nje ya wakati na mdhamini wake uhusiano wao sio wa moja kwa moja.

(v) Muombaji wa usajili nje ya wakati hakusoma Skuli.

(vi) Muombaji anaomba cheti cha Kifo nje ya wakati.

(vii) Muombaji aliyefika umri wa kuanzia miaka 18 anataka kubadilisha jina

(viii) Au mazingira mengine yoyote yatakayoonekana yanahitaji uwepo wa hati ya kiapo kama itakavyoelekezwa na Kitengo cha huduma za kisharia.

## 18. NGAZI (RANK) ZA VYANZO VYA TAARIFA KATIKA KUFANYA UCHUNGUZI WA TAARIFA ZA WAOMBAJI WA VYETI VYA KUZALIWA NJE YA WAKATI.

Katika kufuatilia usahihi wa taarifa za Waombaji wa vyeti vya kuzaliwa nje ya wakati mpangilio wa vyanzo vifuatavyo utakuwa ukizingatiwa katika kujiridhisha juu ya usahihi wa taarifa za Muombaji:

(i) Gamba la Kliniki, kwa waombaji watakao kuwa wameambatanisha vivuli vya magamba katika maombi yao.

(ii) Barua ya Skuli ya Msingi, kwa waombaji watakaokuwa wamesoma Skuli na kuambatanisha na Barua hizo.

(iii) Taarifa zilizopatikana katika Kitambulisho cha Taifa-NIDA, kwa waombaji watakao kuwa wameambatanisha kivuli cha kitambulisho hicho.

(iv) Taarifa zilizopatikana katika Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, kwa waombaji watakao kuwa wameambatanisha kivuli cha kitambulisho hicho.

(v) Na taarifa nyengine ambazo zitapatikana kutoka Ofisi ya uchanguzi (kwa waombaji walioambatanisha kadi za kupigia kura) Leseni (kwa waombaji walioambatanisha leseni), Hati ya kiapo (kwa waombaji walioambatanisha hati hizo) Barua ya Sheha au uthibitisho mwengine wowote

**NB**. Afisa Usajili anaweza kufanya usajili wa cheti cha kuzaliwa baada ya kujiridhisha kwa kutumia vyanzo vilivyotajwa hapo juu, na anaweza kutumia chanzo kimoja tu bila ya kwenda kwenye chanzo kingine iwapo atakuwa ameridhika na usahihi wa taarifa kutoka chanzo alichokiamini.

## 19. MAJADWELI YA MALIPO YA HUDUMA ZA USAJILI YA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR

### 19.1 JADWELI LA MALIPO YA USAJILI WA TUKIO LA KIZAZI

| S/N | CHETI | ADA |
|---|---|---|
| 1. | Cheti cha kuzaliwa cha usajili wa ndani ya wakati (siku 42) na kuombwa ndani ya miezi 3. | TSH. 2,500/= |
| 2. | Cheti cha kuzaliwa cha usajili wa ndani ya wakati (siku 42) na kuombwa baada ya miezi 3. | TSH. 7,000/= |
| 3. | Cheti cha kuzaliwa cha nje ya wakati kuanzia siku 43 mpaka mwaka mmoja na miezi 11. | TSH. 22,000/= |
| 4. | Cheti cha kuzaliwa cha nje ya wakati kuanzia miaka 2 – 5 na miezi 11. | TSH. 32,000/= |
| 5. | Cheti cha kuzaliwa cha nje ya wakati kuanzia miaka 6 na kuendelea. | TSH. 42,000/= |
| 6. | Kubadilisha jina katika cheti cha kuzaliwa. | TSH. 30,000/= |
| 7. | Marekebisho ya herufi ya jina au kurekebisha taarifa katika cheti cha kuzaliwa. | TSH. 20,000/= |
| 8. | Kupata cheti kipya baada ya cheti cha awali kuharibika au kupotea. | TSH. 4,000/= |

### 19.2 JADWELI LA MALIPO YA USAJILI WA TUKIO LA KIFO

| S/N | CHETI | ADA |
|---|---|---|
| 1. | Cheti cha kifo cha usajili wa ndani ya wakati (siku 7) na kuombwa ndani ya miezi 3. | TSH. 1,500/= |
| 2. | Cheti cha kifo cha usajili wa ndani ya wakati (siku 7) na kuombwa baada ya miezi 3. | TSH. 3,500/= |
| 3. | Cheti cha kifo cha nje ya wakati kuanzia siku 8 mpaka mwaka mmoja. | TSH. 11,000/= |
| 4. | Cheti cha kifo cha nje ya wakati kuanzia mwaka 1 – 2. | TSH. 20,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Cheti cha kifo cha nje ya wakati kuanzia miaka 2 na kuendelea. | TSH. 50,000/= |
| 6. | Kupata cheti kipya baada ya cheti cha awali kuharibika au kupotea. | TSH. 4,000/= |
| 7. | Kurekebisha taarifa katika cheti cha kifo. | TSH. 20,000/= |
| 8. | Kubadilisha jina katika cheti cha kifo. | TSH. 30,000/= |

### 19.3 JADWELI LA MALIPO YA USAJILI WA TUKIO LA NDOA

| S/N | CHETI | ADA |
|---|---|---|
| 1 | Cheti cha ndoa. | TSH. 20,000/= |
| 2 | Marekebisho ya taarifa katika cheti cha ndoa. | TSH. 20,000/= |
| 3 | Kupata cheti kipya baada ya cheti cha awali kuharibika au kupotea. | TSH. 20,000/= |

### 19.4 JADWELI LA MALIPO YA USAJILI WA TUKIO LA TALAKA

| S/N | CHETI | ADA |
|---|---|---|
| 1. | Cheti cha talaka. | TSH. 20,000/= |
| 2. | Marekebisho ya taarifa katika cheti cha talaka. | TSH. 20,000/= |
| 3. | Kupata cheti kipya baada ya cheti cha awali kuharibika au kupotea. | TSH. 20,000/= |

### 19.5 JADWELI LA MALIPO YA USAJILI WA KITAMBULISHO CHA MZANZIBARI MKAAZI

| S/N | KITAMBULISHO | ADA |
|---|---|---|
| 1. | Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kwa muombaji asiyezidi miaka 25. | Bure (hakilipiwi) |
| 2. | Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kwa muombaji mwenye umri zaidi ya miaka 25. | TSH. 20,000/= |
| 3. | Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kilichopotea kwa mara ya kwanza au kuharibika. | TSH. 20,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kinachohitaji marekebisho kwa mara ya pili. | TSH. 30,000/= |
| 5. | Kurekebisha taarifa katika kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. | TSH. 20,000/= |

## 20. HITIMISHO

Muongozo huu utatumika pamoja na Sheria No.3 ya mwaka 2018, Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na Kanuni zake (Kanuni za wakala wa usajili wa matukio ya kijamii za mwaka 2020 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2021, Sheria No. 5 ya mwaka 1985, Sheria ya Mzanzibari pamoja na marekebisho yake No.4 ya mwaka 2003, sambamba na Sera ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi za mwaka 2007. Muongozo huu utakuwa ni kisaidizi katika masuala mbalimbali ya usajili wa matukio ya kijamii Zanzibar.

Muongozo huu umetolewa na Uongozi wa Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, utaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2022. Na utadumu kwa muda wa miaka miwili (2) na kuweza kufanyiwa marekebisho.

**………………………**

**MOHAMED A. MAKAME**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII**
**ZANZIBAR**

CENTER FOR YOUTH
DIALOGUE